# Mwongozo wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii (ESMF) na Mwongozo wa Michakato wa Usimamizi (PF).

Mradi wa Mifumo ya Chakula, Matumizi Endelevu ya Ardhi na Maji, pamoja na Urejesho wa Mandhari ya Misitu nchini Tanzania.

## Utangulizi

FOLUR ni Mradi wa Mifumo ya Chakula, Matumizi Endelevu ya Ardhi na Maji, pamoja na Urejesho wa Mandhari ya Misitu nchini Tanzania (*Food Systems, Land Use and Restoration in Tanzania's Forest Landscapes - FOLUR*) unatekelezwa katika Halmashauri ya Mlimba Mkoani Morogoro (Tanzania Bara) na Halmashauri ya Kaskazini A na Kaskazini B Mkoa wa Kaskazini kwa upande wa Zanzibar. Lengo kuu la mradi ni kukuza mbinu jumuishi zinazochanganya uzalishaji endelevu wa chakula kwa kuimarisha minyororo ya thamani isiyochochea uharibifu wa misitu hususan zao la mpunga, pamoja na mipango ya utunzaji na urejeshaji wa mandhari, ili kulinda na kuendeleza mifumo ya ikolojia.

Mradi wa FOLUR unafadhiliwa na Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF), huku Shirika la Uhifadhi wa Mazingira Duniani (WWF) likiwa ndio taasisi inayosimamia utekelezaji wa mradi na Idara ya Misitu na Nyuki chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii ndio mtekelezaji. Kwa muktadha huo, Mwongozo wa WWF wa Kinga za Mazingira na Jamii (SIPP) unatumika katika mradi huu. Mwongozo huu unataka kuandaliwa kwa Mwongozo wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii (ESMF) pamoja na Mwongozo wa Mchakato wa Usimamizi (PF).

## MALENGO YA MIONGOZO HII - ESMF NA PF

**Mwongozo wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii (ESMF):** Lengo la ESMF ni kuainisha misingi, taratibu, na hatua za kutambua na kupunguza athari hasi za kimazingira na kijamii zinazohusiana na mradi. Hatua hizi zinazingatia sheria na kanuni za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (URT) pamoja na Viwango vya Kinga za Mazingira na Jamii vya WWF (ESSF). Kwa kuwa upeo kamili wa shughuli zitakazotekelezwa utajulikana tu wakati wa awamu ya utekelezaji, athari mahususi za kijamii na kimazingira katika maeneo husika hazijulikani kwa sasa. Hivyo, uandaaji wa Mipango Mahususi ya Usimamizi wa Mazingira na Jamii (ESMPs) kwa kila eneo hauwezekani kwa sasa. ESMF inahitajika ili kuweka taratibu za awali za kushughulikia athari hasi za kijamii na kimazingira zinazoweza kujitokeza. ESMPs za maeneo mahususi zitaundwa kulingana na mwongozo huu wa ESMF wakati wa utekelezaji wa mradi.

**Mwongozo wa Michakato wa Usimamizi (PF):** Mradi huu unahusisha Kiwango cha WWF cha Vikwazo/Zuio la Matumizi ya Rasilimali na Uhamishaji wa Makazi. Hii ni kwa sababu mradi unaweza kuzuia au kuathiri utumiaji wa maliasili na shughuli za kujitafutia riziki za watu wanaoguswa au kuathiriwa na shughuli na maamuzi ya mradi (*Project Affectec Persons - PAP*). Mwongozo huu wa Michakato (PF) unaelezea jinsi jamii husika zitakavyoshiriki katika kutambua, kubuni, kutekeleza, na kufuatilia shughuli za mradi pamoja na hatua za upunguzaji wa athari. Lengo la PF hii ni kuhakikisha ushiriki wa Watu Wanaoguswa au Kuathiriwa na Mradi (PAP) huku ikitambua na kulinda maslahi yao, na kuhakikisha kuwa hali zao za maisha hazizoroteki kutokana na mradi huu.

## METHODOLOJIA ILIYOTUMIKA KUANDAA MIONGOZO

Miongozo hii yani ESMF/PF iliandaliwa kupitia njia zifuatazo:

- **Mapitio ya nyaraka**: Sera za SIPP za WWF na sheria za mazingira na jamii za Tanzania (URT).

- **Mashauriano ya kijamii**: Majadiliano na wadau 136 (Ngazi ya Halmashauri na Kijiji/Shehia) ambayo yalifanyika kati ya kipindi cha Septemba na Oktoba 2020.
- **Ujumuishaji**: Miongozo ya ESMF na PF zimeunganishwa kuwa hati moja ili kurahisisha rejea.

### Malengo na Vipengele vya Mradi

Lengo kuu la mradi ni kukuza mbinu jumuishi zinazochanganya uzalishaji endelevu wa chakula kwa kuimarisha minyororo ya thamani isiyochochea uharibifu wa misitu hususan zao la mpunga, pamoja na mipango ya utunzani na urejeshaji wa mandhari, ili kulinda na kuendeleza mifumo ya ikolojia nchini Tanzania hususan kwenye Kongani za Kilimbero na Zanzibar.

Mradi umeratibiwa katika maeneo manne:

- **Kipengele cha 1**: Usimamizi jumuishi wa ardhi (ILM), mipango ya matumizi endelevu ya ardhi, na maji.
- **Kipengele cha 2**: Ukuzaji wa mifumo endelevu na jumuishi ya uzalishaji wa mpunga.
- **Kipengele cha 3**: Uhifadhi, utunzaji, na urejeshaji wa uoto asilia kwa ushirikiano wa jamii na sekta binafsi.
- **Kipengele cha 4**: Uratibu, ufuatiliaji, na tathmini ya mradi (M&E).

### Maeneo ya Mradi (Wasifu wa Eneo)

Mradi unatekelezwa katika maeneo mawili makuu:

I. **Kongani ya Kilombero (Tanzania Bara)**
- Ipo Wilaya ya Kilombero, Halmashauri ya Mlimba
- **Ukubwa**: Hekta 1,356,130 (ardhi oevu na tambarare ya mafuriko makubwa ya maji baridi) **Mwinuko**: Mita 210 hadi 250 juu ya usawa wa bahari.
- **Mfumo wa Ikolojia**: Sehemu kubwa ni ardhi oevu ya asili yenye mito mingi. Inaunda eneo kubwa zaidi la msimu la nyanda za chini za maji baridi katika Afrika Mashariki.
- **Idadi ya Watu**: Wakazi 407,880.
- **Jamii**: Wenyeji (Wapogoro, Wandamba, Wabena, Wambunga) na wafugaji wa kuhamahama (Wamaasai, Wasukuma, Wabarabaig).

  **Ikumbukwe**: Ijapokuwa makundi haya (Wamaasai, Wasukuma, Wabarabaig) hayapati sifa za upokee (indigeneous people) kwa mujibu wa Katiba ja JMT, lakini yana sifa zinazohitaji umakini na ufuatiliaji wa karibu wakati wa shughuli za mradi ili kuhakikisha ushiriki wao.
- **Uchumi**: Kilimo cha kujikimu cha mpunga na mahindi, uvuvi, na ufugaji.

II. Kongani ya Zanzibar (Zanzibar)
- Inapatikana Wilaya za Kaskazini A na Kaskazini B (Unguja, Zanzibar)
- **Ukubwa**: Hekta 43,100 (ardhi ya chini yenye miinuko midogo na minazi).
- **Idadi ya Watu**: Kaskazini A ina wakazi wapatao 105,880.

- **Jamii**: Washirazi/Waswahili, Watumbatu, na makabila mchanganyiko ya Bantu (Wasukuma, Wanyamwezi, n.k.).
- **Uchumi**: Kilimo ndiyo shughuli kuu ya kiuchumi.

**Kwa Ujumla:** Makundi yenye unyonge/hali duni zaidi (vulnerable groups) kwenye Kongani zote ni pamoja na wanawake hususan wajani na wajawazito, walemavu, vijana, watoto hasa yatima, familia duni, kaya zilizo chini ya wanawake, wazee, na jamii ya wafugaji. Chanzo kikuu cha uduni wao ni ubaguzi wa kijinsia, umri, ulemavu, magonjwa, ukosefu/uduni wa kipato na mitaji, ukosefu wa ajira, na kukosa elimu.

### Sera na Sheria za JMT

- **Sera ya Usimamizi wa Mazingira (Bara)**: Sera ya Taifa ya Mazingira (1997), Mkakati wa Taifa wa Uhifadhi wa Maendeleo Endelevu, na Mpango wa Taifa wa Hatua za Mazingira.
- **Sera ya Usimamizi wa Mazingira (Zanzibar)**: Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Namba 2 (1996), Sheria ya Rasilimali za Misitu Namba 10 (1996), Sera ya Misitu (1995/2013), Sera ya Mazingira (1992/2012), Sera ya Uvuvi, Mpango wa Hatua za Mazingira (ZEAP), Mpango wa Usimamizi wa Misitu (2009-2020), na Makubaliano ya Misitu ya Jamii.
- **Matumizi ya Ardhi (Bara)**: Sera ya Taifa ya Ardhi (1995), Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Namba 6 (2007), na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 4 (1999).
- **Matumizi ya Ardhi (Zanzibar)**: Inasimamiwa na Kamisheni ya Ardhi.
- **Upatikanaji wa Ardhi na Fidia**: Mradi hautafanya unyakuzi wa ardhi wala kuhamisha makazi. Iwapo kutakuwa na shughuli zitakazo athiri maisha ya watu (PAP), fidia itatolewa kulingana na Sheria ya Ardhi Namba 4 (1999) Kifungu cha 156 (Bara) na Sheria ya Umiliki wa Ardhi (1992) Kifungu cha 5(4) (Zanzibar).
- **Ushirikishwaji wa Jamii**: Unasisitizwa na sera mbalimbali za sekta za mazingira, ardhi, kilimo, umwagiliaji, maji, na misitu nchini Tanzania.
- **Wenyeji Asilia (*Indegeneous People*s)**: Tanzania haitambui kisheria uwepo wa wenyeji asilia (*indigenous peoples*), ingawa ina makabila 125-130. Kuna makabila machache yanayoonekana kuwa nyuma Zaidi kimaendeleo ikiwa ni pamoja na Wahadzabe, Wabarabaig, Wasandawe, na Wamaasai. Kwa mujibu wa Katiba ya JMT, Makabila yote yana haki sawa ya kupata na kutumia rasilimali.

### Viwango vya Kinga vya WWF

Viwango hivi vinataka athari zote mbaya ziepukwe au zipunguzwe. Viwango vinavyotumika ni:

- Viwango vya Usimamizi wa Athari za Mazingira na Jamii
- Viwango vya Ulinzi wa Mazingira ya Asili
- Uhamishaji Makazi wa Lazima
- Viwango kuhusiana na Wenyeji Asilia
- Viwango vya Afya, Usalama, na Ulinzi wa Jamii
- Viwango vya Usimamizi wa Visumbufu (Wadudu na Magugu)

- Viwango vya usimamizi wa Rasilimali za Kitamaduni
- Viwango vya Mfumo wa Uwajibikaji na Malalamiko
- Viwango vya Mashauriano na Umma na Uwekaji Wazi
- Viwango vya Ushirikishwaji wa Wadau

## MAPENGO KATI YA SHERIA ZA JMT NA SIPP YA WWF

Mifumo hii miwili inaendana kwa kiasi kikubwa, lakini ina utofauti ufuatao:

- **Athari za Mazingira**: SIPP ya WWF ina mahitaji mapana zaidi. Inataka uchambuzi wa kina wa mazingira na jamii ufanyike kabla ya kuidhinisha shughuli yoyote au kutoa fedha.
- **Haki za Fidia**: Sheria za JMT zinajali tu watu wenye hati miliki au haki rasmi za matumizi ya ardhi. SIPP ya WWF inataka watumiaji wote wa ardhi (hata wasio na hati miliki) wapewe msaada au fidia kama maisha yao yataathiriwa na mradi.
- **Mashauriano ya Jamii**: SIPP ya WWF inahitaji mashauriano ya kina na ya lazima wakati wa kuandaa nyaraka za kinga na utekelezaji wa mradi. Sheria za JMT hazina msisitizo mkubwa wa kisheria kwenye jambo hili.

**Angalizo la Utekelezaji**:
Mradi huu unaongozwa na sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT) na Sera ya Kinga ya Mazingira na Jamii (SIPP) ya WWF. Ikitokea utofauti, kanuni za SIPP za WWF zitatumika.

## USIMAMIZI NA UTEKELEZAJI

Idara ya Misitu na Nyuki (DFoB) ya Wizara ya Maliasili na Utalii (MNRT) itakuwa Wakala Mkuu wa Utekelezaji, ikitekeleza Mradi huu kwa niaba ya Wizara ya Fedha na Mipango, ambaye ni Mpokeaji.

Washirika wakuu wa utekelezaji wa FOLUR wanajumuisha Kitengo kikuu cha Usimamizi wa Mradi (PMU), Kilichopo Jengo la Wizara ya Maliasili na Utalii – Idara ya Misitu na Nyuki (MNRT- DFoB), na pia kuna Ofisi ya uratibu kwa kila Kongani (LCU) kwa ajili ya Kilombero na Unguja mtawalia.

- **PMU**: Itahusika na usimamizi na utekelezaji wa kila siku wa mradi.
- **LCUs**: Zitasimamia utekelezaji katika ngazi ya mandhari ya wilaya.
- **Kilombero LCU**: Itakuwa chini ya Halmashauri ya Mlimba Wilaya ya Kilombero.
- **Unguja LCU**: Itakuwa chini ya MANRLF/DFNR.
- **Project Steering Committee** (PSC): Kamati ya Uendeshaji ya Mradi itakayoongozwa na Katibu Mkuu wa MNRT. Itatoa usimamizi mkuu na mwongozo wa kimkakati wa mradi.
- **LAC**: Jukwaa lililopo la Wadau Wengi wa Kilombero litafanya kazi kama Kamati ya Ushauri ya Mandhari. Itasaidia Kilombero LCU katika mikakati, mpango kazi, na utekelezaji. Itahakikisha usambazaji mpana wa taarifa kwa washirika wa mradi.
- **WWF GEF Agency**: Kama Wakala wa Utekelezaji wa GEF, itatoa usimamizi wa kiufundi na kifedha. Itasaidia masuala yanayoathiri utekelezaji wa mradi kwa wakati na kwa ubora.

- **Mtaalamu wa ESS**: PMU itaajiri Mtaalamu wa Usalama wa Mazingira na Jamii. Atawajibika kwa Mkurugenzi wa PMU na kutoa msaada wa usalama kwa PMU na LCUs zote mbili.

**Mifumo ya Usalama (Safeguards)**
Taratibu maalum na majukumu yanayohusiana na utekelezaji wa mahitaji ya usalama wa mazingira na jamii, kama ilivyoelezwa katika ESMF/PF hii ni kama ifuatavyo:

**Wakala Mkuu wa Utekelezaji (MNRT/DFoB)**
**Wajibu**: Anabeba wajibu mkuu wa kuhakikisha mifumo ya usalama wa mazingira inatekelezwa.

**Kamati ya Uendeshaji ya Mradi (PSC)**
**Wajibu**: Usimamizi mkuu na ufuatiliaji wa uzingatiaji wa ahadi za usalama. Kutoa msaada na mapendekezo maalum kuhusu masuala ya usalama ikihitajika.

**Wakala wa WWF GEF (WWF GEF Agency)**
**Wajibu**: Usimamizi mkuu na ufuatiliaji wa uzingatiaji wa miongozo na taratibu za usalama. Kutoa msaada na mapendekezo maalum kuhusu masuala ya usalama ikihitajika.

**Kitengo cha Usimamizi wa Mradi (Pmu)**

**Nyaraka**: Kuhakikisha nyaraka za zabuni na mikataba zinajumuisha vipengele maalum vya usalama wa mazingira na jamii.
**Usimamizi**: Kutekeleza na kusimamia ESMF na mipango mingine ya usalama.
**Ripoti**: Kutoa ripoti za usalama kwa Wakala wa Utekelezaji.
**Uratibu**: Kusimamia mtaalamu wa ESS na kutoa msaada kwa LCUs.
**GRM**: Kutekeleza Utaratibu wa Kushughulikia Malalamiko (GRM).
**Utoaji Taarifa**: Kusambaza (*disclosure and dissemination*) nyaraka za usalama na kuripoti utekelezaji kwa PSC, WWF, na GEF.

**WARATIBU WA LCU**

**Uzingatiaji**: Wanabeba wajibu mkuu wa kuhakikisha uzingatiaji wa Mifumo ya Usalama ya ESMF na viambatisho vyake.
**Uchunguzi**: Kuchuja shughuli zote za mradi ili kubaini athari za kijamii na kimazingira.
**Nyaraka**: Kuchangia katika maandalizi ya nyaraka za usalama (ESMPs za eneo maalum au LRPs) kama inavyotakiwa.
**Mikataba**: Kuhakikisha mahitaji ya usalama yanajumuishwa kwenye nyaraka za zabuni na mikataba yote ya mradi.
**Ushauri**: Kusimamia uzingatiaji wa wakandarasi na kufanya mikutano ya ushauri na wadau wa ndani.
**Ukaguzi**: Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa maeneo ya mradi na kuripoti kwa mtaalamu wa ESS na Mkurugenzi wa PMU.

**GRM**: Kuhakikisha utekelezaji wa GRM na kusambaza taarifa za malalamiko kwa jamii za kwenye maeneo yao ya utekelezaji.

**MTAALAMU wa ESS**

**Uchambuzi**: Kupitia mipango ya kazi na bajeti za kila mwaka ili kubaini viashiria na vihatarishi vya usalama.
**Usaidizi**: Kusaidia Waratibu wa LCU katika kutekeleza miongozo ya usalama na uchunguzi wa shughuli za mradi.
**Maandalizi**: Kuandaa na kuchangia katika nyaraka za usalama kwa ushirikiano wa karibu na PMU na LCUs.
**Ushirikishwaji**: Kuhakikisha mashauriano na jamii yanajumuisha kila mtu/kundi na yanarekodiwa vizuri.
**Ufuatiliaji**: Kufanya ziara za uwandani ili kufuatilia uzingatiaji wa miongozo ya ESMF/PF.
**GRM**: Kuendesha Utaratibu wa Kushughulikia Malalamiko (GRM) wa mradi.
**Ujuzi**: Kutoa msaada wa uwezo wa kiufundi kwa PMU, LCUs, na wadau wengine wa mradi kuhusiana na masuala ya Jinsia, Usalama wa Mazingira na Jamii.
**Utoaji Ripoti**: Kuripoti utendaji mzima wa usalama kwa PSC, WWF GEF Agency, na wadau wengine.

**Athari za Mazingira Zinazotarajiwa na Hatua za Kuzipunguza**
Mradi wa FOLUR unalenga kuimarisha mifumo ya chakula hususan kilimo cha zao la mpunga, na uhifadhi wa mazingira katika maeneo ya mradi, na hivyo unatarajiwa kuleta matokeo chanya na makubwa ya kimazingira. Hata hivyo, athari hasi za mazingira ambazo ni ndogo na za eneo husika pekee zinaweza kujitokeza na zinategemewa kujumuisha yafuatayo.

**Shughuli Lengwa Chini ya Matokeo ya mradi namba 2.2.2: Mikakati ya kipaumbele ya mnyororo wa thamani endelevu katika sekta ya uzalishaji wa mpunga iliyopangwa kutekelezwa.**
Matokeo haya yanajumuisha mfululizo wa shughuli zinazostahili ambazo zinaweza kusababisha athari mbaya za mazingira, kama ilivyoonyeshwa kwenye Jedwali la 1 hapa chini.

**Jedwali la 1: Athari mbaya za mazingira chini ya Matokeo 2.2.2**

| Kipengele | Shughuli Zinazoweza Kufanyika | Athari Hasi Zinazoweza Kutokea kwa Mazingira | Hatua Zinazopendekezwa za Kupunguza Athari |
|---|---|---|---|
| **Pembejeo za Kilimo** | Utambulisho wa mbegu bora za mpunga kupitia Kituo cha Utafiti wa Kilimo na Mbegu cha Tanzania na TARI.<br>Uhamasishaji wa mifumo ya viuatilifu na mbolea ambayo ni salama zaidi kwa mazingira. | Mbegu mpya zinasababisha uharibifu wa udongo na mimea ya asili ya eneo husika, kupunguza rutuba ya udongo, n.k.<br>Viuatilifu na mbolea vinatumika isivyostahili na kuharibu udongo, kusababisha madhara kwa mimea ya asili na viumbe visivyokusudiwa, kuzalisha | Tathmini ubora wa mbegu kwa kuzingatia anuai ya viumbe (biodiversity), matumizi mazuri ya maji, na hali ya eneo.<br>Hakikisha ni mbegu zinazoendana tu ndizo zinazopandwa.<br>Jenga uwezo wa washirika wa utekelezaji ili kuhakikisha uelewa kamili |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | taka, na vinaweza kusababisha uchafuzi wa kupitiliza (eutrophication) kwenye vyanzo vya maji vya chini. | na maarifa kuhusu matumizi na athari za viuatilifu na mbolea zilizochaguliwa. Hakikisha hakuna uharibifu wa bahati mbaya unaosababishwa kwa mimea ya asili au viumbe visivyokusudiwa. |
| **Kwenye Shamba** | Kujaribu mbinu za uzalishaji wa mpunga zinazotumia maji kwa ufanisi, uboreshaji wa usawazishaji wa mashamba, ukarabati/uundaji na uendeshaji wa miundombinu sahihi ya uingizaji na uondoaji maji mashambani.<br><br>Kujaribu mbinu zilizoboreshwa za usimamizi wa rutuba ya udongo.<br><br>Kuhamasisha uvunaji wa maji ya mvua na umwagiliaji wa kisasa kupitia msaada wa kiufundi na kutoa ruzuku kwa miundo mbinu midogo. | Athari zinazohusiana na ujenzi (k.v., uchafuzi wa mazingira, vumbi, kelele, taka, n.k.) zinazotokana na uchimbaji, usimamizi wa taka na vifaa kwenye eneo la mradi.<br><br>Uharibifu wa udongo na/au madhara kwa mimea ya asili.<br><br>Taka ngumu kama vile makapi/pumba za mpunga. | Hatua za kimfumo za kudhibiti usumbufu wa kelele, kusimamia usombaji na ukusanyaji wa taka, kuzuia uchafuzi wa vumbi na kuchafuliwa kwa maji, n.k.<br>Kuchukua hatua za kuzuia mmomonyoko wa udongo, maporomoko ya ardhi, na mafuriko. |
| **Shughuli za Baada ya Kuvuna** | Kufadhili ujenzi wa miundo mbinu ya kuhifadhia mazao baada ya kuvuna.<br><br>Kutumia tena taka za makapi/pumba za mpunga kutengeneza mkaa mbadala (briquettes) ambao ni rafiki kwa mazingira, vifaa vya ujenzi, au chakula cha mifugo. | Athari zinazohusiana na ujenzi (k.v., uchafuzi wa mazingira, vumbi, kelele, taka, n.k.) zinazotokana na uchimbaji, usimamizi wa taka na vifaa kwenye eneo la mradi.<br><br>Uharibifu wa udongo na/au madhara kwa mimea ya asili. | Angalia maelezo yaliyo hapo juu (hatua za kudhibiti kelele, vumbi, taka, na mmomonyoko). |

## Shughuli Zinazostahili Chini ya Matokeo 3.1.1: Urejeshaji wa Ardhi Iliyoharibika katika Maeneo ya Kipaumbele kwa Mujibu wa Mipango ya Mandhari

Athari hasi za kimazingira zinazoweza kutokea kutokana na shughuli hii ni pamoja na teknolojia za urejeshaji wa ardhi zinaweza kuathiri vibaya maeneo ya vyanzo vya maji, mifugo, na uoto wa asili. Athari hizo zinaweza kujumuisha upandaji wa spishi vamizi ili kuboresha ardhi iliyoharibika, uharibifu wa makazi asilia ya viumbe hai, matumizi yasiyo

sahihi ya kemikali za kilimo kutokana na uelewa mdogo wa wakulima kuhusu matumizi salama ya viuatilifu, na ukataji wa miti na mimea ambao unaweza kuathiri vibaya mfumo wa ikolojia (kwa mfano kupungua kwa maeneo ya malisho).

**Hatua za kupunguza athari hizi ni pamoja na:**

- Kutathmini kufaa na kuendana kwa spishi zinazopandwa kwa kuzingatia bioanuwai, matumizi ya maji, hatari za moto wa misitu, mahitaji ya jamii, na masuala ya kitamaduni.
- Kuhakikisha kuwa spishi za asili pekee ndizo zinazopandwa.
- Kutekeleza hatua za kuzuia uchimbaji mkubwa wa udongo na kelele ili kupunguza athari kwa makazi asilia.
- Kutoa mafunzo na kujenga uwezo kuhusu matumizi na utunzaji salama wa viuatilifu.
- Kuhakikisha kuwa hakuna uharibifu wa bahati mbaya kwa uoto wa asili.
- Kutambua maeneo mbadala ya malisho ya mifugo.

**Athari za Kijamii Zinazotarajiwa na Hatua za Kuzipunguza**

Mradi unatarajiwa kuleta matokeo chanya ya kijamii kwa kuboresha maisha ya wananchi wa vijijini, kuimarisha ustahimilivu wa jamii dhidi ya mabadiliko ya tabianchi, na kuwezesha ushiriki wa jamii katika usimamizi wa rasilimali za asili.

Athari hasi za kijamii zinatarajiwa kuwa ndogo na maalum kwa maeneo husika, na zinaweza kujitokeza chini ya matokeo 1.1.3, 2.2.2 na 3.1 ya mradi.

**1. Migogoro ya Kijamii**
Migogoro inaweza kutokea kuhusu vigezo vya uchaguzi wa vijiji lengwa (Kilombero) na katika uandaaji wa mipango ya usimamizi katika maeneo yote mawili.

**Hatua za kupunguza:**
- Shughuli zinazoweza kusababisha migogoro kati ya jamii au kati ya wakulima na wafugaji zifanyike baada ya mashauriano na watu wote wanaoweza kuathirika.
- Mipango ya usimamizi wa jamii iandaliwe kwa njia shirikishi, jumuishi na ya mashauriano.
- Mabadiliko yoyote ya mipaka yafanyike baada ya mashauriano ya awali na ridhaa ya jamii husika pamoja na mamlaka zinazohusika.
- Endapo mabadiliko ya mipaka yataathiri vyanzo vya kipato au maisha ya watu, fidia kamili na kwa wakati itolewe kwa watu wote walioathirika kwa mujibu wa Mpango wa Urejeshaji wa Maisha (*Livelihood Restoration Plan - LRP*).
- Kufanyika kwa kampeni za uhamasishaji na mafunzo kuhusu haki na kanuni za usimamizi wa ardhi na malisho.

**2. Vizuizi vya Upatikanaji wa Rasilimali za Maisha**

Baadhi ya mipango ya usimamizi wa shughuli za mradi inaweza kuzuia matumizi ya rasilimali na vyanzo vya kipato kama vile maeneo ya malisho au vyanzo vya maji ya umwagiliaji.

**Hatua za kupunguza Athari:**

- Kaya zote, wafugaji na wakulima - wafugaji watakaopoteza au kuzuiwa tutumia rasilimali kutokana na mradi watapatiwa msaada wa kurejesha maisha yao.
- Waratibu wa LCU kwa ushirikiano na Mtaalamu wa Masuala ya Jinsia, Usalama wa Jamii na Mazingira wa PMU watafanya uchunguzi wa shughuli zote zilizopangwa ili kubaini uwezekano wa kuwepo kwa vizuizi vya utumiaji wa rasilimali.
- Endapo kaya zilizoathirika zitabainika, tathmini ya kijamii itafanyika kwa kushirikisha jamii husika.
- Kwa kuzingatia matokeo ya tathmini hiyo, Mpango wa Urejeshaji wa Maisha (LRP) utaandaliwa kwa kushirikisha wadau wote ili kutoa msaada mahsusi wa kiuchumi kwa watu walioathirika.

**3. Afya na Usalama Mahali pa Kazi na Katika Jamii**

Kwa mfano, ubora na upatikanaji wa maji unaweza kuathirika, na shughuli za ujenzi zinaweza kuleta hatari za usalama au matumizi ya kemikali hatarishi.

**Hatua za kupunguza:**

- Waratibu wa LCU na wakandarasi watahakikisha mazingira salama na yenye afya kwa wafanyakazi na jamii.
- Hatari za kimwili, kemikali na kibaolojia zitadhibitiwa.
- Mahitaji maalum ya wanawake yatazingatiwa katika hatua zote za utekelezaji.

**Taratibu za Kutambua na Kusimamia Athari za Kimazingira na Kijamii**

Shughuli zifuatazo hazitafadhiliwa chini ya Mradi wa FOLUR:

1. Shughuli zinazohusisha ununuzi au matumizi ya viuatilifu vya daraja la IA, IB au II kwa mujibu wa WHO.
2. Shughuli zinazohitaji ununuzi wa ardhi binafsi.
3. Shughuli zinazohitaji watu kuhamishwa kutoka makazi au biashara/shughuli zao halali.
4. Shughuli zinazohusisha ukataji wa miti katika maeneo nyeti ya hifadhi na vyanzo muhimu vya maji.
5. Shughuli za uchimbaji wa mawe au madini.
6. Shughuli za ukataji miti kwa madhumuni ya biashara.

**Kabla ya kuanza shughuli yoyote ya mradi:**

- Waratibu wa LCU watajaza fomu ya uchunguzi wa ustahiki na athari za mazingira na jamii (*Safeguards Eligibility and Impacts Screening*).

- Ikiwa uchunguzi utaonesha haja ya tathmini zaidi au mwongozo wa ulinzi wa mazingira na jamii vifanyike/viandaliwe, tathmini hizo zitafanywa kabla ya shughuli kuanza.
- Ikiwa athari hasi zitabainika, Mpango wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii (ESMP) utaandaliwa na Mtaalamu wa ESS kwa kushirikiana na Mratibu wa LCU.

**Mwongozo ya Kuandaa Miongozo ya Usimamizi wa Mazingira na Jamii wa eneo husika (ESMP).**

ESMP inapaswa kuandaliwa kabla ya kuanza kwa shughuli husika.

Mpango huo unapaswa:

- Kueleza athari hasi zinazotarajiwa.
- Kubainisha hatua za kuzuia au kupunguza athari hizo.
- Kueleza utaratibu wa utekelezaji, majukumu ya taasisi mbalimbali, mawasiliano, mashauriano na utoaji wa taarifa.

**Ufuatiliaji (*Monitoring*)**
**Ngazi ya Mradi**
PMU ina jukumu la jumla la kusimamia utekelezaji wa ESMF na kufuatilia uzingatiaji wa masharti yote ya mazingira na jamii.

**Ngazi ya Shughuli za Uwandani**
Waratibu wa LCU watafuatilia shughuli zote za mradi na kuhakikisha zinazingatia ESMF pamoja na masharti yaliyotolewa na mamlaka za Tanzania. LCU pia zitawajibika kuhakikisha wakandarasi na watoa huduma wote wanazingatia matakwa ya ESMF, PF na ESMP.
**Ngazi ya Taasisi za Utekelezaji**
WWF kama taasisi ya kuangalia utekelezaji na Wizara ya Maliasili na Utalii (MNRT) kama taasisi ya usimamizi wa mradi zina jukumu la kuhakikisha uzingatiaji wa ESMF.

**Ushirikishwaji wa Jamii Wakati wa Utekelezaji wa Mradi**

Mbali na hatua zilizobainishwa katika Mpango wa Ushirikishwaji wa Wadau (SEP):

- Jamii zinazoathiriwa zinapaswa kushirikishwa kabla ya utekelezaji wa shughuli yoyote inayoweza kuathiri maslahi, haki au maisha yao.
- Ikiwa uchunguzi utaonyesha uwepo wa athari hasi, mashauriano ya jamii yatafanyika kabla ya shughuli kuanza.
- Shughuli zinazoweza kusababisha upotevu au vikwazo vya maisha lazima ziambatane na Mpango Maalum wa Urejeshaji wa Maisha (LRP).

Watu wanaopaswa kushirikishwa ni wale ambao:

- Wanaweza kupoteza mali zao au haki ya kutumia mali au rasilimali za jamii na za asili; au
- Wanaweza kupoteza chanzo cha kipato au njia ya kujikimu, hata kama hawatahamishwa kimakazi.

Makundi maalum yanayopaswa kushirikishwa kikamilifu ni:

- Wanawake (hasa wajane na kaya zinazoongozwa na wanawake)
- Vijana
- Watu wenye ulemavu
- Wazee
- Makundi ya wafugaji wanaohamahama kama Maasai na Barabaig katika mandhari ya Kilombero.

Ili kuhakikisha ushirikishwaji ni jumuishi, taarifa zifikishwe kwa wadau kupitia njia mbalimbali kama matangazo, redio za kitaifa, televisheni na mbinu nyingine za mawasiliano zinazofaa.

**Utatuzi wa Malalamiko**

Mfumo wa Utatuzi wa Malalamiko (GRM) wa FOLUR utasimamiwa na kuratibiwa katika ngazi ya Makao Makuu – PMU. Kwangazi ya Uwandani/Kongani, ofisi za Kongani zitaratibu mfumo kwa kusaidia uwasilishaji wa malalamiko ngazi ya PMU. Mtaalamu wa ESS (PMU) atakuwa na jukumu la uendeshaji wa GRM katika PMU na kila LCU itamteua mtu mmoja atakayewajibika kukusanya na kushughulikia malalamiko yanayohusu shughuli katika kila maeneo yake ya utendaji. Mwongozo wa uendeshaji wa GRM umeainishwa kwenye ESMF (Mfumo wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii).

**Uwekaji Wazi (Disclosure)**

Jamii zote zitakazoathiriwa na shughuli za mradi pamoja na wadau wote kwa ujumla watafahamishwa kuhusu mahitaji na majukumu ya ESMF kulingana na vigezo vilivyoainishwa kwenye ESMF.

Wakati wa utekelezaji wa FOLUR, ESMPs (Mipango ya Usimamizi wa Mazingira na Jamii) mahususi kwa kila shughuli zitaandaliwa kwa kushauriana na jamii zilizoathirika na kuwekwa wazi kwa wadau wote kabla ya kukamilisha wazo la mradi.

**Bajeti**

Gharama za utekelezaji wa EMSF, ikiwa ni pamoja na gharama zote zinazohusiana na fidia kwa watu walioathiriwa na mradi, zitagharamiwa kikamilifu kutoka kwa bajeti ya FOLUR. Itakuwa ni jukumu la PSC (Kamati ya Kuelekeza Mradi) na PMU kuhakikisha kuwa kuna bajeti ya kutosha kwa ajili ya hatua zote mahususi za upunguzaji athari zinazoweza kuhitajika kwa kuzingatia EMSF.